

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

### TANGAZO LA AJIRA YA MUDA MFUMO WA ANWANI ZA MAKAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya anapenda kuwatangazia nafasi 233 za ajira za muda kwa ajili ya kuingiza taarifa za majengo, viwanja na maeneo ya huduma kwenye mfumo wa NaPA katika kata, vijiji na vitongoji vyote vilivyopo wilaya ya Chunya. Malipo kwa siku ni shilling elfu ishirini tu (20,000/=)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe Raia wa Tanzania kuanzia umri wa miaka 18-40
2. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
3. Awe anamiliki na kujua kutumia vizuri simu janja yenye teknolojia ya android na yenye kukaa na chaji angalau siku moja (saa 24)
4. Awe na barua pepe inayofanya kazi/active
5. Awe mkazi wa kata/kijiji/kitongoji husika

#### KAZI NA MAJUKUMU YA MWOMBAJI

1. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, wategemezi, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa National Physical Addressing (NaPA)
2. Kutuma taarifa ulizokusanya kila siku umalizapo kazi kwenye mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA)

#### KUMBUKA

##### Maombi yaambatanishwe na:

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
3. Picha (Passport size) mbili
4. Nakala ya vyeti vya taaluma

##### NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe zikiwa na anwani kamili ya mwombaji ikiwa ni pamoja na **barua pepe** na **namba ya simu**. Maombi yawasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Chunya kwa anwani ya S.L.P 73 CHUNYA kupitia kwa watendaji wa kata husika. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14.03.2022 saa 9:30 alasiri.

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya.

Tamim H. Kambona  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
CHUNYA  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHUNYA

Itigi Road, S.L.P73, Chunya simuyamezani: 025 2520121, Barua pepe: [ded@chunyadc.go.tz](mailto:ded@chunyadc.go.tz),  
tovuti: [www.chunyadc.go.tz](http://www.chunyadc.go.tz)